RIPOTI YA KAMATI YA MAWASILIANO NA UJENZI YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Kamati ya Mawasilino na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi ni moja wapo ya Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi iliyoanzishwa kwa Kifungu cha 85 cha Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984 na Kanuni ya 106(d) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2012. Kazi na majukumu ya Kamati hii yamebainishwa na kufafanuliwa kwenye Kanuni ya 111 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi kama ifuatavyo:-

a) Kufuatilia utekelezaji wa Maagizo ya Kamati yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia.

b) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji wa Bajeti na hotuba nyengine za Waziri alizotowa katika Baraza.

c) Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na Miradi ya Wananchi katika Wizara husika.

d) Kuchunguza na kufuatilia Mapato na Matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha.

e) Kuchambua Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Wizara husika ya Mapato na Matumizi ya kila mwaka.

f) Kushughulikia Miswada ya Sheria inayokabidhiwa kwake na Spika.

g) Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekeleaji wa ahadi hizo.

h) Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

i) Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ambapo katika ripoti hii inajulikana kama “Kamati” inawajibu wa kufuatilia utekelezaji wa Wizara mbili za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ikiwa ni pamoja na Idara, Mashirika, Mamlaka na Vitengo vilivyo chini ya Wizara hizo. Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii ni kama zifuatazo:-

1) Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira

2) Wizara ya Ujenzi, Mawasilino na Usafirishaji

1.1 WAJUMBE WA KAMATI

Kamati hii inaundwa na Wajumbe wafuatao:-

1.	Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Suleiman Sarhan Said	-	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Mjumbe
4.	Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Mjumbe
5.	Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Mjumbe
6.	Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali	–	Mjumbe
7.	Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	-	Mjumbe
8.	Mhe. Nassor Salim Ali	-	Mjumbe
9.	Mhe. Said Omar Said	-	Mjumbe
10.	Ndg. Fatma Omar Ali	-	Katibu
11.	Ndg. Himid Haji Choko	-	Katibu

1.2 MALENGO YA KAZI NA MUDA WA KAZI ZA KAMATI

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Kamati ilitekeleza kazi zake kwa malengo yafuatayo:-

a) Kufuatilia Maagizo yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka 2013/2014.
b) Kufuatilia ahadi za Serikali zilizotolewa katika Mkutano wa Bajeti wa mwaka 2015/2016.
c) Kufuatilia utekelezaji wa Bajeti (kazi za kawaida na kazi za maendeleo) ya mwaka 2015/2016.
d) Kufuatilia ukusanyaji wa mapato katika vitengo vya Serikali pamoja na kufanya ziara katika taasisi husika.

Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Kamati ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki sita kama ifuatavyo:-

1) Unguja, kuanzia tarehe 29/08/2016 hadi tarehe 02/09/2016 na terehe 05/09/2016 hadi tarehe 13/09/2016 kwa upande wa Pemba.

2) Unguja, kuanzia tarehe 31/10/2016 hadi tarehe 11/11/2016.

3) Unguja kuanzia tarehe 16/1/2017 hadi tarehe 20/1/2017 na tarehe 23/1/2017 hadi tarehe 27/1/2017 kwa upande wa Pemba.

Aidha, Kamati kwa kushirikina na Wizara husika ilibahatika kutembelea Tanzania Bara pamoja na Mombasa Kenya ili kujifunza kwa vitendo na hatimae kuweza kuishauri Serikali ipasavyo. Kamati ilitembelea Bandari ya Tanga na Dar es - Salaam, kituo cha Umeme Rasi Kiromoni kilichopo Tanzania Bara pamoja na kufanya ziara ya mafunzo katika Bandari ya Mombasa.

Pia, katika kuhakikisha ufanisi wa Masuali mbali mbali yanayogusa Wizara zinazosimamiwa na Wizara hii, Kamati iliwakutanisha Viongozi wa Wizara ya Fedha na Uchumi, Mfuko wa Barabara, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji na Viongozi wa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kukwamua ujenzi wa barabara ya Mwanakwerekwe - Fuoni. Vile vile, Kamati ilifanikiwa kusafiri kwenda Tanzania Bara kukutanana na Uongozi wa Wizara ya Fedha na Mipango wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Uongozi wa TANESCO ili kuzungumzia suala la deni la Umeme la Zanzibar pamoja na Madeni ya Umeme ya Taasisi za Muungano zenye Ofisi zao hapa Zanzibar.

Aidha, Kamati ilikutana na Waziri mwenye dhamana ya Masuala ya Muungano pamoja na Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti na Usafiri wa Baharini (SUMATRA) ili kuzungumzia changamoto zinazogusa Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati Zanzibar (ZURA) pamoja na Mamlaka ya Usafiri wa Baharini Zanzibar (ZMA).

1.3 HADIDU REJEA

Katika Utekelezaji wa kazi kwa mwaka 2016/2017, Kamati ilitumia hadidu rejea zifuatazo:-

a) Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984.
b) Kanuni za Baraza La Wawakilishi, Toleo la mwaka 2012.
c) ‘Hansard’ za Baraza za mwaka 2015/2016,
d) Ripoti za Kamati kwa Mwaka 2013/2014
e) Hotuba za Bajeti za Taasisi za Serikali zinazosimamiwa na Kamati hii.

SEHEMU YA PILI

WIZARA YA ARDHI, MAJI, NISHATI NA MAZINGIRA

2.0 UTANGULIZI

Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ni Wizara mama katika Mfumo wa utoaji wa huhuma za kijamii kwa wananchi wa Zanzibar. Aidha, Wizara hii ina dhamana ya kuhakikisha kwamba wananchi wote wanafaidika na huduma bora za maji, matumizi bora ya ardhi, usimamizi na utunzaji wa mazingira pamoja na upatikanaji bora wa nishati iliyo salama na endelevu kwa ustawi wa maisha yao.

Wizara hii imeundwa na sekta kuu tano ambazo ni Mipango, Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

2.1 SEKTA YA MIPANGO NA UENDESHAJI

Sekta hii imegawika kama ifuatavyo:-

a. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.
b. Idara ya Utumishi na Uendeshaji.
c. Afisi Kuu Pemba.

Kamati imegundua kwamba jukumu kubwa la sekta hii ni kuratibu na kusimamia Sera, Mipango na Shughuli zote za kawaida na za maendeleo za Wizara husika.

2:2 CHANGAMOTO

Ufinyu wa Bajeti; Idara hizi licha ya kubeba jukumu la uendeshaji wa Wizara nzima lakini bajeti inayotengewa ni finyu hali inayopelekea baadhi ya shughuli kutokutekelezwa ipasavyo kama zilivyopangwa.

2:3:0 SEKTA YA ARDHI

Sekta ya Ardhi ndani ya Wizara hii imeundwa kwa Idara na Taasisi zifuatazo:-

a. Idara ya Ardhi na Usajili (Mahakama ya Ardhi, Afisi ya Mrajis wa Ardhi na Bodi ya Uhaulishaji).
b. Idara ya Upimaji na Ramani.
c. Idara ya Mipango Miji na Vijiji.
   Idara na Taasisi hizo kwa pamoja zinaunda Kamisheni ya Ardhi inayoongozwa na Katibu Mtendaji.

2.3 .1 IDARA YA ARDHI

Kamati imegundua kwamba dhamana kubwa ya Idara hii ni kusimamia Utawala na Usimamizi wa Ardhi kwa lengo la kuhakikisha usalama wa umiliki, kutayarisha hati za umiliki wa matumizi ya ardhi, kuandaa mikataba ya ukodishwaji ardhi pamoja na mikataba ya ardhi maalum kwa ajili ya kilimo (Eka tatu).

Aidha, wakati wa kazi za Kamati, Kamati hii ilitembelea Makao Makuu ya Idara hii pamoja na sehemu mbali mbali mbazo idara inahusika kufanya kazi.

Pamoja na hayo, Kamati imefahamishwa kwamba katika kipindi cha miaka minne iliyopita, jumla ya mikataba 215 ya ukodishwaji ardhi ilitiwa saini na kupewa wawekezaji mbali mbali. Kamati imebaini kwamba miongoni mwa mikataba hiyo ni kama ifuatayo.-

i. 94 ni kwa ajili ya Mahoteli.
ii. 6 ni kwa ajili ya vituo vya Mafuta (Petrol Station).
iii. 1 kwa ajili ya Mradi wa kuwekea wanyama (Zoo).
iv. 21 kwa ajili ya Minara ya Mawasilino ya Simu za Mikononi.
v. 20 kwa ajili ya Makaazi (Resedential).
vi. 1 kwa ajili ya Sea Fuming.
vii. 1 kwa ajili ya Mifugo.
viii. 1 kwa ajili ya Kiwanja cha kufurahishia watoto.
ix. 1 kwa ajili ya Ghala.
x. 2 kwa ajili ya Mradi wa Golf.
xi. 6 kwa ajili ya Viwanda.
xii. 1 kwa ajili ya Skuli.

2:3. 2 MAHAKAMA YA ARDHI

Mahakama ya Ardhi imeanzishwa ikiwa na lengo kuu la kupokea, kusikiliza na kuamua kesi mbali mbali zinazohusu migogoro ya Ardhi. Hadi kufikia Disemba 2016 wakati Kamati ilipotembelea, jumla ya kesi 548 zilikua zikiendelea katika Mahakama hiyo Unguja na Pemba.

2.3.3 MRAJIS WA ARDHI

Afisi ya Mrajis wa Ardhi ni Taasisi iliyoanzishwa ikiwa na lengo la kusajili ardhi na kuweka kumbukumbu ya uhaulishaji wote unaofanywa katika ardhi iliyosajiliwa. Mpaka Kamati inapokea taarifa ya Msajili wa Ardhi, jumla ya maeneo 5000 yalikuwa yameshasajiliwa Unguja na Pemba.

2.3.4 IDARA YA UPIMAJI NA RAMANI

Idara hii ina jukumu kubwa la kupima, kutengeneza ramani, kuendeleza ukusanyaji na uwekaji wa kumbukumbu za taarifa za msingi za ardhi zinazotokana na Upimaji na Ramani ambazo zitasaidia mfumo wa usajili Ardhi Unguja na Pemba. Aidha, Kamati imegundua kwamba katika kipindi cha miaka mitano iliyopita jumla ya Viwanja 1,741 vilipimwa ikiwemo vya Makaazi (979), Huduma (91), Vitega Uchumi (101), Taasisi (126) na mashamba (444).

2.3.5 IDARA YA MIPANGO MIJI NA VIJIJI

Idara hii ndio chombo pekee chenye dhamana ya upangaji wa matumizi bora na endelevu ya ardhi kwa miji, vitongoji na vijiji. Kamati imebaini kwamba licha ya uchanga wa Idara hii kwa

kipindi cha miaka mitano yaani 2015/2020, idara inakusudia kupanga miji midogo 14 Unguja na Pemba pamoja na kupanga maeneo ya wazi zaidi ya 15 kwa mji wa Zanzibar.

2:3: 4 CHANGAMOTO ZINAZOZIKABILI IDARA YA ARDHI, MAHAKAMA YA ARDHI, MRAJIS WA ARDHI, IDARA YA UPIMAJI NA RAMANI PAMOJA NA IDARA YA MIPANGO MIJI NA VIJIJI

Kwa ujumla changamoto zinazozikabili taasisi zote zilizo chini ya Kamisheni ya Ardhi ni kama zifuatavyo:-

1. Kukosekana kwa mfumo wa uhakika wa usajili wa ardhi, jambo ambalo linafanya utambuzi na usajili wa ardhi kusitasita.

2. Kuwepo kwa migogoro sugu ya ardhi ambayo inachukua muda mwingi wa watendaji.

3. Kuchelewa kufanyiwa mapitio kwa sera ya ardhi.

4. Upungufu wa wataalamu hasa wenye utaalamu wa utawala, usimamizi na uthamini, usajili na utambuzi wa ardhi, nyenzo na vitendendea kazi.

5. Kuchelewa kwa upimaji wa viwanja na utoaji wa hati baada ya upimaji.

6. Uchakavu wa jengo la Afisi Kuu ya Mahakama ya Ardhi liliopo Vuga pamoja na uhaba wa vyoo.

7. Madeni ya Wazee wa Mahakama Unguja (Accessors).

8. Uelewa mdogo wa jamii juu ya masuala ya usajili wa Ardhi hali inayopelekea zoezi la usajili kutokuenda kwa haraka.

9. Ukosefu wa ujuzi wa kutosha wa masuala ya utambuzi na usajili wa Ardhi kwa watendaji wa Afisi hiyo.

2:3: 5 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira iwe na Chanzo Kimoja (kitengo) tu cha kusajili Ardhi katika taasisi zake zinazohusiana na masuala ya ardhi.

2. Kamati inaomba Kamisheni ya Ardhi iandae mpango maalum wa kuwapatia mafunzo ya masuala ya ardhi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ikiwemo masuala ya upimaji, usajili, utambuzi, umiliki na matumizi ya Ardhi.
3. Kamati pia inaiomba Kamisheni ifanye Utafiti Maalum kuangalia mahitaji ya wananchi juu makaazi ili kuondokana na Migogoro mtambuka ya ardhi.

4. Kamati inaiomba Serikali pamoja na Wizara kwa ujumla kuipatia Mahakama ya Ardhi jengo jengine la kufanyia kazi ili kunusuru afya za wafanyakazi wake kutokana na uchakavu wa jengo linalotumika hivi sasa.

5. Vile vile, Kamati inaiomba Wizara iharakishe kuyapima maeneo yanayotengwa kwa ajili ya shughuli za Maendeleo na Miradi ya Maendeleo na wahusika kupatiwa Hati ili kuepusha uvamizi wa sehemu hizo.

6. Kamati inaitaka Wizara impatie eneo jengine Mmiliki wa FK Interprise Company ili kupisha mradi mkubwa wa uwekezaji ambao uko tayari kuanza katika eneno la uwekezaji huko Nungwi.

2.4 : 0 SEKTA YA MAJI

2.4.1 MAMLAKA YA MAJI (ZAWA)

Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) imeanzishwa chini ya Sheria ya Maji Namba 4 ya Mwaka 2006 kama ilivyopendekezwa katika Sera ya Maji ya Taifa ya Zanzibar ya Mwaka 2004, ikiwa na jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama pamoja na kulinda na kuhifadhi rasilimali maji.

Kamati imegundua kwamba pamoja na jitihada mbali mbali za Serikali, Viongozi wa majimbo na wafadhili kulivalia njuga suala la upatikanaji wa maji safi na salama, bado kuna mapungufu ya kutokuwepo uwiano kati ya maji yanayozalishwa na yale yanayohitajika. Hadi Kamati inaandaa taarifa hii, hali ya uzalishaji na mahitaji ya maji ilikua kama ifuatavyo:-

SN	MKOA	MAHITAJI (Litre/day)	UZALISHAJI (Litre/day)	UPUNGUFU (Litre/day)
1.	M /MAGHARIB	82,206,212	66,968,184	15,938,028
2.	M/KUSINI- U	19,112,905	14,403,350	4,709,555
3.	M/KASK- U	32,902,523	20,945,976	11,263,547
4.	M/KASK- P	47,674,864	28,186,800	19,488,064
5.	M/KUSN- P	46,812,926	31,022,759	15,790,167
	JUMLA	228,716,430	161,527,068	67,189,361
	%		**70.6%**	**29.4%**

Kutokana na hali hiyo, Kamati imebaini kwamba suala la upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi bado imekuwa ni changamoto kubwa inayokosa ufumbuzi wa uhakika. Vile vile, Kamati imebani changamoto nyengine inayoikabili Mamlaka ya Maji kuwa na deni linalodaiwa hasa na Shirika la Umeme pamoja na Madeni kwa wateja wake ambayo kwa kiasi kikubwa yanarejesha nyuma utendaji wa mamlaka hiyo. Hadi Kamati inaandaa Ripoti hii, ZAWA ilikua inadaiwa deni la umeme Tsh **15,999,062,028.38** linalotokana na vituo vya uzalishaji wa maji na **Tsh 1,962,426,428.44** yanayotokana na wasambaji (Suppliers). Aidha, ZAWA ilikua ikiwadai wateja wake jumla ya Tsh. **8,378,846,275.07** ambazo zimegawanyika kwa wateja wa majumbani, wateja wa kibiashara, wateja wa taasisi na kilimo kama inavyoonekana katika Jeduweli ifuatayo:-

S/N	AINA YA MTEJA	DENI
1.	MAJUMBANI (DOMESTIC)	6,746,542,359.8
2.	BIASHARA (COMMERCIAL)	1,152,194,121.62
3.	TAASISI (INSTITUTION)	398,229,667.6018
4.	UMWAGILIAJI (AGRICULTURE)	81,880,126.67
	JUMLA	**8,378,846,275.07**

2. 4. 2 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI MAMLAKA YA MAJI ZAWA

1. Ongezeko la Mahitaji: Kutokana na ukuaji wa Maendeleo na ongezeko la idadi ya watu pamoja na ukuaji wa shughuli nyengine za kijamii mijini na vijijini, mahitaji ya maji yamekuwa yakiongezeka kwa kasi kubwa na hivyo kukosekana kwa uwiano kati ya maji yanayozalishwa na mahitaji halisi ya maji.

2. Uchakavu wa Miundombinu: Sehemu kubwa ya mtandao wa mabomba ni ya zamani na machakavu ambao kwa sasa hauwezi kuhimili msukumo wa maji na kusababaisha kiasi cha asilimia 30 % ya maji kupotea njiani kabla ya kuwafikia watumiaji kutokana na uchakavu wa miundombinu hiyo.

3. Mabadiliko ya tabia nchi: Hali ya uzalishaji wa maji imekua ikipungua sana kutokana na mabadiliko ya Tabia nchi yanayosababisha kupungua kwa mvua na rasilimali ya maji ardhini.

4. Muitikio mdogo wa wananchi juu ya uchangiaji wa huduma ya Maji kwa hiari.

5. Uvamizi wa viazio vya maji hali inayopelekea kupungua kwa kasi rasilimali ya maji.

6. Kuongezeka kwa ujenzi wa nyumba usiofuata taratibu za mipango miji.

7. Uvamizi wa maji Chumvi katika vianzio vya maji.

2.4.3 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaiomba Mamlaka ya Maji (ZAWA) ifanye uhakiki wa kutosha na kukagua upotevu wa maji kutokana na uchakavu wa miundombinu yake na baadae kutoa ripoti kwa wadau wote ikiwemo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

2. Kamati inaendelea kuishauri Mamlaka ya Maji (ZAWA) kuweka Afisa husika wa maji katika kila jimbo ambaye atafuatilia vizuri na kwa ukaribu zaidi masuala yote yanayohusiana na maji katika jimbo husika.

3. Kamati inaitaka Mamlaka ya Maji (ZAWA) iendelee kudhibiti uvamizi wa vianzio vya maji kwa kuviwekea vizuwizi (uzio) na matangazo yanayokataza ujenzi, uchimbaji wa mchanga kiholela hali amabayo husababisha uharibufu wa mazingira katika sehemu hizo.

4. Kamati inaiomba Mamlaka ya Maji (ZAWA) kufikiria kuazisha huduma ya kuchangia maji kwa njia ya simu za mkononi ili kuweza kurahisisha huduma ya ulipaji maji na kudhibiti mapato yatokanayo na huduma hiyo kwa Unguja na Pemba.

5. Kamati inaishauri Mamlaka ya Maji (ZAWA) kushirikiana kikamilifu na Viongozi wa Majimbo au wafadhili wanaotaka kuazisha miradi ya maji kwa kutoa ushauri wa kitaalamu kabla ya kuazishwa kwa miradi hiyo.

6. Aidha, Kamati inaiomba Mamlaka ya Maji (ZAWA) kuhakikisha inayapima na kutafuta hati miliki za maeneo yote ya vianzio vya maji Unguja na Pemba.

2.5:0 SEKTA YA NISHATI

2.5.1 SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR (ZECCO)

Shirika la Umeme Zanzibar (ZECCO) ni miongoni mwa taasisi muhimu katika kuunga mkono jitihada za Serikali ya kuwapatia huduma ya umeme wananchi wake na hivyo kuinua hali na kuongeza uchumi wa taifa. Shirika hili linajukumu la kusambaza na kuimarisha hali ya upatikanaji bora wa huduma ya Umeme wa uhakika Mijini na Vijijini.

2.5.1. CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR

1. Ongezeko la madeni kwa tasisi za serikali: Hadi Kamati inatayarisha ripoti hii, Shirika lilikua linazidai taasisi za Serikali (SMT na SMZ) **Tsh.** 22,990,749.81 kama inavyojionyesha hapo chini:-

S/N	TAASISI	DENI (TZS)
1.	MAMLAKA YA MAJI - ZAWA	16,937,916,982.39
2.	TAASISI NYENGINE - SMZ	4,397,152,751.70
3.	TAASISI ZA SMT	1,655,680,057.72
	JUMLA	**22,990,749,791.81**

2. Shirika linaendelea kutumia mfuko wake kwa kazi za kusambaza umeme vijijini, kazi ambayo kikawaida ilitakiwa kufanywa na Serikali Kuu au mfuko maalum kwa ajili ya kazi hiyo.

3. Shirika linakabiliwa na deni kubwa la ununuzi wa umeme kutoka Tanesco, deni ambalo limefikia TZS 63 Bilioni hadi 2016. Deni ambalo linarudisha nyuma maendeleo ya Shirika kiujumla.

2.5.2 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaiomba Shirika la Umeme (ZECCO) kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Maji , Nishati na Mazingira izungumze na Wizara ya Fedha na Mipango kwa lengo la kuweka utaartibu wa malipo ya umeme kuingizwa moja kwa moja katika Account za ZECCO badala ya kuingizwa katika OC za Taasisi husika.

2. Kamati inaendelea kulishauri Shirika la Umeme (ZECCO) kuongeza ulinzi katika Vituo vyake vyote vya Uzalishaji na Usambazaji umeme hususan katika maeneo ya Fumba, Mtoni pamoja na Rasi Kiromoni.
3. Kamati vile vile inaliomba Shirika la Umeme (ZECCO) kufanya utaratibu wa kuyapima na kuyatafutia hati miliki maeneo yote ya vianzio na vituo vya umeme kwa Unguja na Pemba.

2.5.3 IDARA YA NISHATI NA MADINI

Idara ya Nishati na Madini imeanzishwa kwa uwezo wa Rais wa kuanzisha taasisi ikiwa na jukumu la kusimamia rasilimali za nishati na madini na huduma zake.

Aidha, Mradi wa Nishati Mbadala Zanzibar (Zanzibar Renewable Energy Project) ni miongoni mwa miradi ya Idara hii. Mradi wa Nishati Mbadaka (uliofungiwa mkataba mwezi Februari 2014) unafadhiliwa na Umoja wa nchi za Ulaya ambapo jumla ya Euro Milioni tatu (Euro 3,000,000) zitatumika kwa miaka mitatu kutekeleza mradi huo.

Lengo kuu la Mradi huo ni kuangalia uwezekano wa kuzalisha umeme hapa Zanzibar kwa kutumia Nishati Mbadala (solar anda wind). katika utekelezaji wa Mradi huo, vipimo vya mwenendo wa upepo na upatikanaji wa jua vinatarajiwa kukusanywa na kufanyiwa kazi ili kujua ni kiwango gani cha umeme kinaweza kuzalishwa hapa Zanzibar kwa kutumia nishati hiyo. Hivyo, maeneo yaliyojengwa minara hiyo ni Makunduchi, Mbuyu Tende na Bambi kwa Unguja na Mwambe, Micheni pamoja na Kiuyu-Maziwa Ngombe kwa Pemba. Hata hivyo, Kamati haijaridhiswa sana na mwenendo wa mradi huo ambao unaonekana kusuasua katika hatua za utekelezaji wake.

2.5.4. Mafuta na Gesi Asilia

Kamati inaipongeza Wizara kwa kuandaa Sheria ya Utafutaji na Uchimbaji Mafuta na gesi Asilia hapa Zanzibar ikiwa na lengo la kusimamia, kulinda na kudhibiti suala zima la uchimbaji na upatinaji wa mafuta na gesi asili hapa Zanzibar.

Aidha, Sheria hiyo imepitishwa na Baraza la Wawakilishi tarehe 27/10/2016 na kuwekwa saini na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi mnamo tarehe 15/11/2016. Pia, Kamati imepata taarifa kwamba tayari Wizara imeshawasilisha Mpango kazi wa suala hilo Baraza la Mapinduzi ambapo hatua za kuazishwa kwa Kampuni ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPDC) na Mamlaka ya Usimamizi wa Utafutaji na Uendelezaji wa Mafuta na gesi Asilia (ZPRA) zimo katika Mamlaka ya uteuzi wa Viongozi.

Vile vile, Kamati imegundua kwamba tayari kumekuwa na mazungumzo ya kuelewana na Mamlaka husika ya Tanzania Bara kuhusiana na Usimamizi wa Vitalu vinavyopakana na Tanzania Bara.

2:5:5 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI IDARA YA NISHATI NA MADINI

1. Zanzibar kutokuwa na chanzo cha umeme wake na hivyo kutegemea chanzo kimoja tu cha umeme kutoka Tanzania Bara.

2. Uhaba wa wataalamu wa masuala ya Mafuta na Gesi Asilia hapa nchini.

2.5.6 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaiomba Idara ijiandae vyema katika kuwaanda wafanyakazi wake katika usimamizi wa fani ya mafuta na gesi asilia.

2. Pia, Kamati inaitaka Idara ianze mchakato wa kuwaajiri vijana walioko masomoni wanaosomea fani ya Mafuta na Gesi ili iwadhibiti mapema kwa manufaa ya Taifa.

3. Kamati inaiomba Wizara kwa kushirikiana na Idara ya Nishati na Madini kuendelea na hatua ya kutoa elimu kwa wananchi, ili waweze kuelewa umuhimu na faida ya rasilimali hiyo.

4. Kamati inaitaka Serikali kwa kushirikiana na Wizara kuharakisha uanzishwaji wa Taasisi pamoja na Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Mafuta na Gesi Asilia kama Sheria inavyoelekeza.

2.5.7 MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR (ZURA)

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) imeanzishwa chini ya Sheria Namba 7 ya mwaka 2013. Aidha, Nishati zinazosimamiwa na Mamlaka ni Umeme, Mafuta, Gesi Asilia na Nishati nyengine yoyote inayozalisha umeme. Pia, katika sekta ya Maji, Mamlaka inasimamia udhibiti wa maji safi na maji machafu.

2:5: 8 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA YA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR (ZURA)

1. Kutokuwepo kwa mfumo huru wa uingizaji nishati ya mafuta na kusababisha nishati hii kuwa ghali, pamoja na uchakachuaji na magendo ya mafuta.
2. Kukosekana kwa hifadhi ya Serikali ya Mafuta.
3. Mgongano wa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Maji na Nishati (ZURA) na Sekta nyengine zikiwemo zinazodhibitiwa kama vile Umeme na Maji.
4. Tozo la ada ya Bandari huko Dar es Salaam kwa mafuta yanayokuja Zanzibar kuwa kubwa tofauti na yale yanayokwenda nchi jirani ambayo hutozwa Dollar 3 kwa kila lita moja wakati yanayokuja Zanzibar hutozwa Dollar 10 kwa lita moja.
5. Uhaba wa wafanyakazi: Mamlaka bado haijapata wafanyakazi wa kudumu walioajiriwa kwa ajili ya kufanya kazi za Mamlaka. Hali hii imeilazimu Mamlaka kuchukuwa wafanyakazi kutoka Idara na Taasisi nyengine za Serikali.

6. Ukosefu wa Afisi ya Kudumu ya Mamlaka: Afisi za Mamlaka zipo katika jengo la Mfuko wa Barabara kwa Unguja lakini bado idadi ya Vyumba havitoshi katika uwezo wake wa kiutumishi.
7. Kukosekana kwa Afisi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA) huko kisiwa Pemba.

2:5: 9 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka kubadilisha Mfumo wa uagiziaji na uingizaji wa mafuta nchini kwa kutumia mfumo wa Uagiziaji wa pamoja.
2. Kamati inaiomba Serikali pamoja na Wizara husika kuanzisha ujenzi wa miundombinu ya mafuta ikiwemo Bandari na Bohari ya Mafuta hapa nchini.
3. Kamati inaiomba Wizara kuzifanyia mapitio Sheria zote za sekta zinazodhibitiwa na Mamlaka hii ili ziende sambamba na majukumu ya ZURA yaliopangwa kwa mujibu wa Sheria husika.
4. Kamati inaitaka Wizara iipatie ZURA eneo la ujenzi wa Ofisi zake za kudumu ili kupunguza gharama wanazoendelea kuzilipa kutokana na kodi ya pango.
5. Kamati inaiomba Serikali kuanzisha utaratibu wa kuweka ‘Reserve Tank’ ya Mafuta ili iweze kutumika wakati wa Dharura.
6. Kamati inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kuwa na Taasisi moja tu inayoshughulikia masuala ya uchakachuaji na ukusanyaji wa mapato ya mafuta.

2:6: 0 SEKTA YA MAZINGIRA

2:6: 1 MAMLAKA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA NA IDARA YA MAZINGIRA

Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira ina jukumu la kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Miongozi na Viwango nya Mazingira kwa ajili ya kupunguza uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Aidha, kuna mafanikio mengi yamepatikana tangu kuanzishwa kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira pamoja na Idara yake. Miongoni mwa mafanikio ni kufanya operesheni za kusimamia marufuku ya mifuko ya plastiki Unguja na Pemba, kufanya operesheni ya kusimamia Maliasili zisizorejesheka Unguja na Pemba na kufanya ziara za ufuatiliaji wa Kimazingira.

2:6:2 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI MAMLAKA PAMOJA NA IDARA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA

1. Wakurugenzi wawili kutumia Ofisi moja hali ambayo huleta mtafaruku wakati wa utendaji wa kazi zao.
2. Utupaji ovyo wa taka na kusababaisha uchafuzi na uharibifu mkubwa wa kimazingira.
3. Utupaji ovyo wa maji machafu yanayotapishwa kwenye vyoo na makaro katika Manispaa ya Zanzibar hali ambayo hupelekea kuhatarisha afya za wananchi wanaishi karibu na eneo hilo.
4. Uchimbaji ovyo wa mchanga kwenye maeneo mbali mbali ya Mkoa wa Mjini Magharibi.
5. Athari za Mabadiliko ya tabia nchi.

6. Ukosefu wa baadhi ya Miongozo ya Usimamizi wa Mazingira.
7. Uwezo mdogo waa kimazingira wa kusimamia sekta ya mafuta na gesi asilia.
8. Uhaba wa Jengo ambapo hupelekea mpaka wafanyakazi kkukosa hata pakukaa wakati wakiwepo kazini.

2:6: 3 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaiomba Wizara kulitafutia ufumbuzi wa haraka Suala la Wakurugenzi wawili kujibana bana katika Ofisi moja hali inayopelekea kukosekana kwa usiri wa utendaji wa kazi.

2. Kamati inaiomba Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka pamoja na Idara kuhakikisha inaanzisha mradi wa kuhifadhi maji taka ili kuliokoa eneo la Maruhubi linalotumiwa na waanikaji wa madagaa na kuokoa mazingira ya eneo hilo.

3. Kamati inaishauri Mamlaka ishirikiane kikamilifu na wamiliki wa Mradi Mkubwa wa Uekezaji wa Kampuni ya Bakharessa katika eneo la Mtoni ili kuhakikisha kwamba ujenzi huo unazingatia suala zima la mazingira.

4. Kamati inaitaka Mamlaka iandae safari za 'Field Attachment' nchini Norway ili kujiandaa kukabiliana na athari za kimazingira zitakazotokana na maendeleo ya mafuta na gesi asilia hapa nchini.

WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI

2:7:0 UTANGULIZI

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji imepewa jukumu kuu la kusimamia Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji Zanzibar. Kwa mwaka wa 2016/2017, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu yake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo (Vission 2020), MKUZA III, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015-2020, Sera ya Usafiri Zanzibar (2008), Sera ya TEHAMA, Sera ya Taifa ya Nyumba, na Mpango Mkuu wa Usafiri (Zanzibar Transport Master Plan, 2009) kwa kufuata Bajeti inayotumia programu(PBB).

Programu zinazosimamiwa na Wizara zinatekelezwa kupitia Idara, Mashirika na Mamlaka zifuatazo;-

1. Ofisi Kuu Pemba.
2. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.
3. Idara ya Uendeshaji na Utumishi.
4. Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara.
5. Idara ya Usafiri na leseni.
6. Idara ya Mawasiliano.
7. Mamlaka ya Usafiri wa Baharini.
8. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege.
9. Mamlaka ya Uhifadhi na uendelezaji wa Mji Mkongwe.

10. Shirika la Meli na Uwakala.
11. Shirika la Bandari.
12. Shirika la Nyumba.
13. Wakala wa Majengo.

Katika Ripoti hii, Kamati inaigawa Wizara hii katika Sekta za Utawala, Sekta ya Nyumba, Usafiri wa nchi kavu, Usafiri wa Anga, Usafiri wa Majini na Mawasiliano.

2:7:1 SEKTA YA UTAWALA

Sekta hii inaundwa na Ofisi kuu Pemba, Idara ya Mipango na Utumishi na Idara ya Utumishi na Uendeshaji. Jukumu kubwa la Sekta hii ni Kusimamia masuala ya kiutumishi, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa upande wa Unguja na Pemba.

Aidha, Sekta hii pia inaratibu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kupitia programu zake nne kama ifuatavyo:-

1. Programu ya Miundombinu na Huduma za Usafiri wa Barabara.
2. Program ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe na Uimarishaji wa Majengo ya Serikali na Binafsi.
3. Program ya Huduma za Technolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).
4. Program ya Mipango na Utawala katika Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

2:7:2 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SEKTA YA UTAWALA

1. Kukosekana kwa mawasiliano mazuri baina ya Idara ya Mawasiliano na Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara wakati wa Ujenzi wa Barabara wakati wa utekelezaji wa Mradi wa Mkongo wa Taifa jambo ambalo limepelekea Mkongo huo kuathirika kwa kukatwa na kusababisha hasara kubwa kwa serikali.

2. Bodi karibu tano katika Wizara hii zimeteuliwa lakini hazina bajeti iliyopangiwa za kuziendesha na kushindwa kufanya kazi zake kama ilivyokusudiwa ikiwemo Bodi yaa Condominium, Bodi ya Usafiri barabarani, Bondi ya Wasanifu , Wahandisi na Wakadiriaji Wa Ujenzi, Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba na Bodi ya Wakandarasi.

2:7:3 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati yangu inaishauri Sekta hii kuhakikisha inasimamia kwa karibu zaidi miradi yote mikubwa ya Wizara hii ili kuokoa fedha za umma.

2. Kamati inaitaka sekta hii kuhakikisha na kusimamia kwa katika Bajeti ya mwaka huu, Bodi zote zilizomo kwenye Wizara hii zinatengewa fedha kwa ajili ya kufanya shughuli zao kama Sheria zinavyotaka.

2:8:1 SEKTA YA NYUMBA

Sekta hii imeundwa na Shirika la Nyumba, Wakala wa Majengo na Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe.

2:8:2 SHIRIKA LA NYUMBA

Shirika la Nyumba la Zanzibar ni taasisi inayojitegemea ambayo inafanyakazi zake kwa mujibu wa Sheria Namba 6 ya mwaka 2014. Sheria hii inaipa mamlaka Shirika la Nyumba la Zanzibar kusimamia na kuratibu masuala yote yanayohusu ujenzi, uuzaji na ukodishaji nyumba za kuishi na za biashara.

Wakati Kamati ilipotembelea Shirika hilo na kutembelea baadhi ya Nyumba za maendeleo za Kilimani, Mtemani, Madungu pamoja na Kengeja, Kamati haikuridhika na hali ya usafi na uchakavu wa Nyumba hizo. Hali ya Nyumba za Kengeja ni ya kutisha kwa usalama wa watu wakati mifumo ya maji machafu imekufa kabisa katika vyumba hizo.

Hata hivyo, Kamati inatoa shukurani maalum kwa Mdhamini wa nyumba za maendeleo Pemba kwa jitihada zake za kuanza majaribio ya kuziokoa nyumba za Madungu na Mtemani. Kwa kweli “Pilot Project” yake kupitia na kufanya baadhi ya marekebisho katika mfumo wa maji machafu katika nyumba hizo ni ya kupigiwa mfano na gharama yake ni nafuu kabisa.

2:8:3 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SHIRIKA LA NYUMBA

Pamoja na Mafanikio makubwa yaliyopatikana na ShIrika hilo, Kamati imegundua Changamoto kadhaa ambazo zinahitaji kufanyiwa kazi ili kuliimarisha zaidi Shirika hilo. Changamoto hizo ni kama zifuatazo:-

1. Shirika limerithi nyumba na majengo ambayo yanahitaji matengenezo makubwa.

2. Kukosekana kwa daftari la Mali za Shirika (Fixed Assert Register).

3. Kukosekana kwa hati Miliki za Shirika kwa Majengo yote ya Serikali.

4. Kukosekana kwa Kanuni za kuisaidia Sheria Nambari 6 ya mwaka 2014, ili ifanye kazi kama ilivyotegemewa.

5. Kukosekana kwa Mpango Mkakati (Strategic Plan) wa utekelezaji wa majukumu ya Shirika kwa mujibu wa Sheria na Sera za Nyumba ya Zanzibar.

6. Kuwepo kwa Uvamizi wa ujenzi katika maeneo ya nyumba za Maendeleo.

2:8:4 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaiomba Wizara kwa kushirikiana na Shirila la Nyumba kuanza kuzifanyia matengenezo nyumba ambazo zinaweza kutengenezeka na baadae kufunga mikataba na wananchi na wafanyabiashara ili kuwakodisha na hatimae kujiongezea mapato.

2. Kamati pia inalitaka Shirika kufanya uhakiki na kuzitambua nyumba zake zote na kuziorodhesha katika daftari la Mali za Shirika (Fixed Assert Register).

3. Kamati inaomba Shirika kutafuta Hati Miliki za Nyumba zake haraka iwekekanavyo ili kuondokana na hali ya udanganyifu kwa baadhi ya wamiliki wa nyumba hizo.

4. Vilevile, Kamati inalishauri Shirika kutenga Bajeti maalum kuongeza bajeti na kuwa bega kwa bega na Mdhamini wa majengo Pemba ili kuhakikisha "Pilot Project" yake ya Usafi inafanikiwa.

5. Kamati inaiomba Wizara ihakikishe inatunga Kanuni haraka ili kusaidia utekelezaji wa Sheria Nambari 6 ya Mwaka 2014. Hali ambayo hupelekea ugumu kwa upande wa Shirika katika kutekeleza majukumu yake.

6. Kamati inaitaka Bodi ya Nyumba ifanye kazi zake kama Sheria inavavyoagiza au Mwenyekiti ajiuzulu kwa kushindwa kazi aliyopewa pamoja na wajumbe wake.

7. Kamati inaishauri Shirika la Nyumba kutafuta aidha wabia au taasisi za kifedha kushirikiana nazo ili kuweza kuwawezesha wananchi kuweza kuwakopesha nyumba au kuwajengea nyumba kwa njia ya mkopo nafuu kama wananvyofanya wenzetu Tanzania Bara.

2:8:5 MAMLAKA YA UHIFADHI NA UENDELEZAJI WA MJI MKONGWE

Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe ina jukumu la Uhifadhi wa Urithi wa Kimataifa wa eneo zima la Mji Mkongwe, ikijumuisha Urithi wa kihistoria wa Majengo, Utamaduni wa asili, Mandhari na vivutio vyengine pamoja na kudumisha hadhi ya Urithi ya Mji Mkongwe duniani.

2:8:6 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI MAMLAKA YA UENDELEZAJI NA UHIFADHI WA MJI MKONGWE

1. Ukosefu wa wataalamu katika fani ya usimamizi wa majengo ya kale (kihistoria).

2. Ufinyu wa bajeti hali ambayo hupelekea kushidwa hata kutekeleza majukumu yanayowakabili kwa wakati.

3. Kutokuwepo kwa ushirikishwaji wa wataalamu wetu wa ndani pale inapotokea miradi ya ujenzi wa Mji Mkongwe.

4. Kuchelewa kwa ukarabati wa Nyumba ya Kihistoria ya Beit El Jaib.

2:8:7 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe ishirikishwe kikamilifu wakati wa kuandaa na kutekeleza Miradi ya ujenzi kuitekeleza miradi hiyo ili kuepusha hasara na usumbufu mkubwa wakati wa utekelezaji wake miradi hasa ya Ujnzi ndani ya hifadhi hiyo.

Kamati inazishauri Taasisi mbali mbali kabla ya kuamua utekelezaji wa miradi ya ujenzi katika eneo la Hifadhi ya Mji Mkongwe lazima kwanza ipelekwe kwenye Kamati ya wataalam wa Mamlaka ya Mji Mkongwe ili kutoa miongozo yenye kufaa.

2. Kamati yangu inaishauri Mamlaka ya Mji Mkongwe kwenda UNESCO ili kwenda kukwamua muongozo wa ukarabati wa jengo la Bait El Ajaib ili kuweza kujengwa na watalii waweze kuja kuangalia pamoja kufanya tafiti zao.

3. Kamati inazitaka taasisi zote zinazomiliki majengo katika maeneo ya Mji Mkongwe kufuata ushauri wa kitaalamu kutoka Mamlaka hiyo pamoja kuitekeleza miongozo hiyo hasa katika kukarabati majengo yao ili kuepusha kupata hasara ya kuanguka kwa majengo hayo jambo ambalo Taifa hupoteza rasilimali watu pamoja na mali zao.

2:9:0 SEKTA YA USAFIRI WA NCHI KAVU

Katika Ripoti hii, Kamati inazijumuisha Idara ya Usafiri na Leseni pamoja na Idara ya Utunzaji na Uendelazaji wa Barabara (UUB) kama ni Sekta moja ya Usafiri wa Nchi Kavu.

2:9:1 IDARA YA USAFIRI NA LESENI

Idara ya Usafiri na Leseni ina jukumu la kusimamia usalama kwa watumiaji wa barabara kwa kuendesha shughuli za ukaguzi wa vyombo vya moto, upasishaji madereva, kusajili vyuo vya udereva na walimu wa skuli za udereva. Aidha, idara pia inatoa ruhusa za usafirishaji wa abiria na mizigo kwa njia ya abiria, kutoa beji za utingo na madereva pamoja na kuendesha na kusimamia Karakana Kuu ya Serikali.

2:9:2 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI IDARA YA USAFIRI NA LESENI

1. Uchakavu wa jengo la Makao Makuu ya Idara lilioko Mwanakwerekwe.

2. Uchakavu wa mitambo iliyopo Karakana na sehemu ya mitambo iliyopo Tibirinzi Pemba na Chumbuni Unguja.
3. Ukosefu wa Utaalamu wa teknolojia mpya ya utengenezaji wa magari kwa upande wa Unguja na Pemba.

4. Kukosekana kwa jengo lenye vifaa vya ukaguzi wa vyombo.

2:9:3 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati haikuridhishwa hata kidogo na mazingira ya jengo la Ofisi ya Idara hiyo na kuitaka Wizara kulipatia ufumbuzi wa haraka iwezekanavyo suala hilo.
2. Kamati inaishauri Idara ifanye Mpango wa kuanzisha Skuli za udereva za Madereva wa Viongozi wa Serikali.
3. Kamati inaiomba Idara ifanye ukaguzi wa mara kwa mara kwa vyombo vya moto vya barabarani pamoja na madereva ili kuisaidia Serikali katika kupunguza idadi ya ajali za barabarani.
4. Kamati inaiomba Wizara kupitia Idara kufikiria kuanzisha utaratibu wa ulipaji wa faini za papo kwa papo kwa kulitumia Jeshi la Polisi kama wakala wa kutekeleza suala hilo kama inavyofanyika huko Tanzania Bara.

5. Kamati inataka Serikali pamoja na Wizara husika kupitia Idara kuangalia uwezekano wa kukataza usafiri wa bodaboda ama kutoa leseni na kuwatambua madereva wa Bodaboda hizo ili kuepusha mlolongo wa malalamiko kuhusiana na usafiri huo hasa wakati wa usiku.

2:9:4 IDARA YA UENDELEZAJI NA UTUNZAJI WA BARABARA (UUB)

Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara ina jukumu la kujenga na kutunza barabara zote zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kama zilivyoainishwa kwenye Sheria ya Barabara ya mwaka 1927, ambayo imefanyiwa marekebisho mwaka 2012 ili barabara zipitike kwa urahisi.

Kamati inaipongeza Idara na Wizara kwa ujumla kutokana na juhudi kubwa za kuimarisha mtambo wa barabara Unguja na Pemba. Kamati ilitembelea miradi mbali mbali ya barabara na kuwashuhudia wafanyakazi wa UUB wakifanya kazi usiku na mchana ili kuhakikisha kwamba miradi hiyo inakamilika.

2:9: 5 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI IDARA YA UENDELEZAJI NA UTUNZAJI WA BARABARA

1. Uchakavu na Uhaba wa zana za kufanyia kazi suala ambalo linapelekea Idara kutokuwa na uwezo wa kufanyakazI zaidi ya moja kwa wakati mmoja.
2. Ukosefu wa wataalamu muhimu sana kwa kazi za barabara kama vile Surveyors, Environmental specials na kadhalika.
3. Bajeti ndogo ya fedha za matengenezo. Hii inatokana na mfuko wa Barabara kuwa na chanzo kimoja tu hadi sasa ambacho ni tozo la shilingi 100 inayotokana na mafuta.
4. Kutokana na uhaba na uchakavu wa zana inakua vigumu kukamilisha mradi husika kwa wakati.
5. Malalamiko mengi ya Waheshimiwa Wajumbe kuhusiana na maeneo yanayotakiwa kufanyiwa matengenezo ya barabara majimboni (Njia za Wananchi).
6. Matumizi makubwa ya ununuzi wa vipuri (spare) na zana.
7. Uvamizi wa maeneo ya hifadhi ya barabara, kuondoa viguzo vya hifadhi vilivyowekwa kwa baadhi ya barabara.
8. Baadhi ya watu kukaidi agizo la Idara ya kusimamisha na kubomoa majengo wanapobainika wanajenga katika eneo la hifadhi ya barabara.
9. Baadhi ya watu kuhujumu samani zilizowekwa barabarani na kwenye madaraja.

2:9:6 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kwa kuwa harakati na mahitaji ya ujenzi na utunzaji wa barabara yanaongezeka kwa kasi mijini na vijijini, ni vyema kwa Wizara ikaagiza zana nyengine mpya za kisasa ili kwenda sambamba na mahitaji ya wakati.

2. Kamati inaiomba Serikali iongeze bajeti ya idara hii kutokana na majukumu yake inayopagiwa kuyatekeleza.

3. Kamati inaitaka Bodi ya Mfuko wa Barabara kuacha urasimu usio na msingi wakati wa Ujenzi wa Barabara kwani husababisha ucheleweshaji wa ukamilishaji wa ujenzi wa Barabara na kusababisha kazi nyingine kukwama au kutojengwa kwa wakati.

4. Kamati inaitaka Idara hii kuwasiliana na Afisi ya Rais Ikulu ili kufuatilia ahadi zote za Rais majimboni na kuzitekeleza ili kuondoa malalamiko ya muda mrefu kuhusu utekelezaji wa ahadi hizo, ingawa kwa upande wa Pemba ahadi hizo hutekelezwa kwa haraka sana tofauti na Unguja.

5. Kamati inaiomba Wizara ifanye mpango wa kuwaingiza katika mfuko wa bima ya afya wafanyakazi wake kwa vile wamekuwa wakifanyakazi katika mazingira magumu na hatarishi kwa afya zao.

6. Kamati inaishauri Idara izidi kutoa taaluma kwa wananchi juu ya matumizi bora ya Barabara pamoja na kuheshimu alama ziliomo ili ziendelee kudumu kwa muda mrefu zaidi.

7. Kamati inaitaka Idara iwasiliane na Manispaa na Halmashauri husika ili kuhakikisha kwamba suala la usafi wa barabari linakuwa endelevu.

8. Barabara ya Fuoni iwekwe taa za Barabarani pamoja kuweka watu maalum kwa ajili ya kuifanyia usafi barabara hiyo.

9. Kamati pia inaitaka Serikali kupitia Idara ya UUB kuwalipa fidia wananchi walioko pembezoni ya Barabara ya Wete Chake ili waanze kuhamisha majengo yao pamoja na vipando vyao kwani fedha hizo tayari tumezitenga kwenye bajet hii tuliyonayo ili wakati wa ujenzi utakapoanza isje kuleta usumbufu kwa wananchi.

10. Kamati yangu inaitaka Serikali kupitia Idara hii kufanya kila jitihada ili kuepuka kuukata Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa ili kuepuka hasara kwa Serikali.

2:10:00 SEKTA YA USAFIRI WA MAJINI

Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi inairipoti Sekta hii kua inajumuisha Shirika la Bandari, Mamlaka ya Usafiri wa Baharini (ZMA) na Shirika la Meli na Uwakala.

2:10:01 SHIRIKA LA BANDARI ZANZIBAR

Kamati inatambua kwamba Shirika la Bandari linajukumu la kuziendesha, kuzisimamia na kuziendeleza Bandari tano za Zanzibar ambazo ni Bandari ya Malindi, Mkokotoni, Wesha, Mkoani na Wete.

Kamati imebaini kwamba baada ya Shirika kupata vifaa vipya na vya kisasa vya kunyanyulia mizigo pamoja na vyombo vya kuhudumia meli, kumekuwa na ongezeko kubwa la idadi ya mzigo wa makontena pamoja na mapato ya Shirika hilo kuongezea kwa kasi kubwa.

2:10:02 MRADI WA BANDARI YA MPIGA DURI

Kamati inapongeza juhudi za Wizara za Mradi wa Bandari ya Mpigaduri unaotegemewa kujengwa katika eneo la Mpigaduri, Maruhubi mjini Zanzibar na kugharimu jumla ya Dola za Kimarekani 231,400,000/=. Mradi huu kwa sasa unasubiri kupata Approval kutoka Exim Bank ya China.

2:10:04 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SHIRIKA LA BANDARI ZANZIBAR

Wakati wa kazi za Kamati, Kamati ilibahatika kuzitembelea bandari zote zilizopo Unguja na Pemba. Aidha, licha ya mafanikio makubwa yaliyopatikana bado kumekuwa na changamoto ambazo zimepelekea kutokufikiwa kwa ufanisi unaostahiki katika utoaji wa huduma. Miongoni mwa Changamoto hizo ni:-

1. Ufinyu wa Gati ya Malindi.
2. Ufinyu wa eneo la kuhifadhia makontena Bandarini Malindi.
3. Madeni sungu kwa taasisi mbali mbali zikiwemo za Serikali, pamoja na kuchelewa kwa malipo ya huduma zinazotolewa kwa baadhi ya Makampuni na Mashirika yakiwemo Azam Marine na Shirika la Meli Zanzibar.
4. Uvamizi wa Maeneo ya Bandari pamoja na Minara ya kuongozea vyombo vya Usafiri wa baharini unaofanywa na wananchi kwa kujenga majengo mbali mbali ya makaazi na biashara.
5. Ukosefu wa hati miliki kwa baadhi ya maeneo ya Bandari.
6. Kuharibika kwa mashine mpya ya kunyanyulia mizigo kabla ya kuanza kazi katika bandari ya Mkoani.
7. Bandari nyingi zinahitaji maboresho ili ziweze kukidhi mahitaji ya ufungaji wa vyombo vinavyoingia bandarini na uhifadhi wa mizigo hasa bandari ya Wesha, na Wete ambazo sio wakati wote vyombo vinaweza kufunga gati.
8. Ukosefu wa ‘Xray machine’ kwa ajili ya Upekuzi katika bandari zote kwa upande wa Unguja na Pemba.

2:10:05 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaiomba Serikali pamoja na Wizara kupitia Shirika lifanye juhudi ya kuyapima na kuyatafutia hati miliki maeneo yote ya Bandari na minara ya kuongozea vyombo vya usafiri wa majini.

2. Kamati inaitaka Shirika la Bandari kushirikiana na TRA kutafuta machine ya X-RAY ili kuweza kukagua mizigo kwa uhakika hapo Bandarini .

3. Kamati pia inaipongeza Wizara kupitia Shirika la Bandari kwa ununuzi wa vifaa vya kisasa huko na kuongeza ufanisi wa kazi huko Bandarini lakini ni vyema mafunzo ya ziada wakapatiwa wanaotumia vyombo hivyo ili kuweza kuishi na kutumika kwa muda mrefu.

4. Kuhusu ujenzi wa Bandari ya Wete Pemba Kamati inapongeza na wazo la Serikali kushirikiana na mwekezaji binafsi kuijenga Bandari hiyo lakini inaitaka Serikali kuhakikisha yeyote atakaetaka kuekeza kwenye ujenzi huo ni lazima udhibiti na matumizi ya Bandari yasimamiwe na Shirika la Bandari.

2:10:06 SHIRIKA LA MELI NA UWAKALA ZANZIBAR

Shirika la Meli na Uwakala limepewa jukumu la kusimamia na kuendesha Meli za Serikali, kutoa huduma bora za usafirishaji wa abiria na mizigo baina ya Visiwa vya Zanzibar na kwengineko na kusimamia biashara ya meli kama mmiliki, dalali, wakala wa Kampuni za meli za kigeni zinazofanya biashara hapa Zanzibar.

2:10:07 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SHIRIKA LA MELI NA UWAKALA ZANZIBAR

1. Shirika la Meli na Uwakala linakabiliwa na uchakavu mkubwa wa meli zake (MV. Maendeleo na MT. Ukombozi) ambazo hivi sasa zina umri wa zaidi ya miaka 30 tangu ziliponunuliwa zikiwa mpya mnamo mwaka 1984. Hali hii inapelekea gharama na huduma za uendeshaji na utunzaji wa meli hizo kuwa kubwa.
2. Kwa upande wa MV Mapinduzi II, changamoto kubwa inayojitokeza ni maumbile ya meli hiyo kushindwa kufanyakazi kwa ufanisi kwa vile milango ya sehemu za Mizigo (Ramps) ipo chini sana kulingana na mgongo wa Gati hivyo kutofanyakazi kwa ufanisi.
3. Hadi Kamati inatayarisha Ripoti hii, uendeshaji wa hesabu ya pamoja (Escrow Account) baina ya Shirika na Wizara ya Fedha ilikua ni changamoto kubwa kutokana na mahitaji yanayojitokeza na taratibu za upatikanaji wa fedha za kuhudumia meli hiyo.

2:10:08 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaiomba Serikali pamoja na Wizara kuangalia uwezekano wa kutafuta meli nyengine ya abiria na mizigo ambayo itaendana na mahitaji ya hivi sasa ya kubeba mizigo na abiria ili kukabiliana vyema na soko katika sekta ya usafiri wa majini.
2. Kamati pia inaiomba Serikali kwa kushirikiana na Wizara pamoja na Shirika liangalie uwezekanao wa kutafuta meli nyengine ya mafuta.
3. Kamati inaendelea kulishauri Shirika liangalie uwezekano wa kuanzisha safari zaidi katika Bandari za Tanga, Mtwara na Comoro kwa usafirishaji wa abiria na mizigo ikiwemo saruji.
4. Kamati imepokea maamuzi ya Serikali kuiuza Meli ya MV Maendeleo na kununua meli nyengine lakini, Kamati inatoa angalizo mapema kua Meli itakayonunuliwa izingatie mahitaji ya abiria na wafanyabiashara.

2:10:09 MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI (ZMA)

Mamlaka ya Usafiri Baharini imeanzishwa chini ya Sheria Namba 3 ya mwaka 2009, ambapo inafanya kazi zake za kila siku chini ya Sheria ya Usafiri wa Baharini ya mwaka 2006. Mamlaka ina jukumu la kusimamia usalama na ulinzi wa vyombo vya baharini pamoja na kusimamia shughuli za ukaguzi na usajili wa meli, utoaji wa lesini za makampuni yanayojishughulisha na huduma za bandari, utoaji wa leseni kwa vyombo vidogo vidogo, utoaji wa hati na vitambulisho vya mabaharia.

Kamati ilitembelea Mamlaka hiyo na kugundua kwamba, Mamlaka tayari imefanikiwa kufungua Ofisi yake Dubai ambayo imesajiliwa kwa jina la “Zanzibar Maritime International Service” ambapo Mamlaka hivi sasa inaendesha wenyewe usajili wa Kimataifa wa “Tanzania International Register of Shipping” wakati hapo awali ikiendeshwa na wakala ambae ni kampuni ya Philtex Corporation Ltd.

2:10:10 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI (ZMA)

1. Tuhuma za kusajili meli za Korea ya Kaskazini kinyume na Azimio la Umoja wa Mataifa namba 2270 (2016).
2. Nchi ya Tanzania kutoridhia mikataba ya kimataifa ambapo inatakiwa iridhiwe Bungeni. Hivyo, hali hii inapelekea meli zilizosajiliwa kupitia "Tanzania International Register of Shipping" kuzuiliwa mara kwa mara zinapotembelea bandari za kigeni kutokana na kuonekana kuwa nchi ya Tanzania haijaridhia mikataba hiyo. Hivyo huwa haikidhi baadhi ya vigezo.
3. Kuchelewa kwa mkataba wa makubaliano kati ya Tanzania na Panama (Bilateral agreement). Tatizo hili limewaathiri mabaharia wetu wanapopanda meli za Panama na hivyo kupelekea mabaharia hao kukosa ajira kwenye meli hizo.
4. Philtex kuendelea kusajili meli na kuendelea kutoa vyeti kwa kutumia usajili wa TZIRS kinyume na utaratibu wa kisheria.

2:10:11 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaiomba Mamlaka ihakikishe kwamba inatoa ushauri wa kutosha kwa Mamlaka zinazohusika, ili mikataba ya kimataifa ya usajili wa meli iwezi kuridhiwa Bungeni.
2. Kamati inaiomba Mamlaka ya Usafiri Baharini ihakikishe kwamba inalisimamia kikamilifu suala la ulanguzi wa tiketi pamoja na tiketi za Mikononi kwani linachangia kwa kiasi kikubwa vyombo vya usafiri kupakia abiria kuliko uwezo walio nao.
3. Kamati inaiagiza Mamlaka ya Usafiri Baharini kuisimamisha haraka iwezekanavyo Kampuni ya "Philtex" kutoa huduma ya usajili wa meli kinyume na taratibu na Sheria za nchi hali ambayo inapelekea kuikosesha mapato Serikali.

2:11:00 SEKTA YA USAFIRI WA ANGA

2:11:01 MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ina lengo kuu la kuvisimamia na kuviendesha Viwanja viwili vya Serikali ambavyo ni Kiwanja cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume, Kisauni na Kiwanja cha Pemba. Aidha, Mamlaka ina jukumu pia la kusimamia usalama kwa safari za abiria na mizigo katika Viwanja vya Ndege vya Serikali pamoja na kutekeleza taratibu za Sheria zote za uendeshaji wa Viwanja kama zinavyoelekezwa na Tanzania Authority (TCAA) na International Civil Organisation (ICAO).

Ingawa katika kipindi cha hivi karibuni, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imefanya mambo mengi ya Maendeleo lakini bado inakabiliwa na changamoto kadhaa ambazo ni:-

1. Jengo Jipya la Abiria (Terminal II)

- Mradi wa jengo Jipya haujajumuisha uchabuzi wa mahitaji halisi ya wafanyakazi wanaohitajika katika uendeshaji wa jengo hilo. Aidha, Mradi umekosa 'Component' ya mafunzo kwa wafanyakazi.
- Kwa mujibu wa uchambuzi uliofanywa na washauri elekezi wa mradi wa jengo jipya, gharama za umeme tu katika jengo hilo inatarajiwa kufikia jumla ya Dola za Kimarekani milioni 1.1 kwa mwaka (sawa na TZS 2.3 bilioni).
- Kamati imebaini kuwa vikao vya kujadili maendeleo ya mradi (site meeting) havikujumuisha thamani za ndani ya jengo hilo.
- Mamlaka imekua ikikosa ushirikiano kutoka kampuni ya mshauri elekezi juu ya ushirikishwaji wa mafundi wa Mamlaka katika ujenzi wa jengo jipya. Hili ni jambo la kuzingatia hususan katika ngazi ya ushirikishwaji wa mafundi hao kwani litaipunguzia Serikali utegemezi wa mafundi kutoka nje wakati mradi utakapokamilika na kuanza kufanya kazi.

2. Uchakavu wa magari ya zimamoto yanayotumika katika Kiwanja cha Ndege cha Pemba.
3. Ukosefu wa kifaa cha kuongezea ndege (ILS).
4. Kukosekana kwa vifaa muhimu katika kiwanja cha ndege cha AAKIA.
5. Tatizo la kujaa kwa maji AAKIA.
6. Tatizo la joto: Kamati imebaini kwamba joto limekuwa jingi kwenye ukumbi wa kuwasili na kuondoka abiria.
7. Mazingira: Tatizo la mwitu kuzunguka ndani na nje ya uwanja ni kumbwa.
8. Upungufu wa Mashine za upekuzi wa mizigo (X-ray machines).
9. Kukosekana kwa 'Transformer' ya Umeme wa uhakika katika Uwanja wa Ndege wa Pemba : Mradi wa uwekaji wa Taa Pemba ulihitaji uwekaji wa 'transformer' kwa ajili ya Uwanja tu na sio kwa huduma nyengine za maeneo ya mji inayozunguka Uwanja. Vile vile, Kamati imebaini kuwa kukosekana kwa 'transformer' hiyo ya Uhakiki hupelekea huduma zinzotolewa katika Kiwanja hicho kusuasua.

2:11:02 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaiomba Serikali pamoja na Wizara kuishirikisha Mamlaka ya Viwanja vya ndege kikamilifu katika hatua zote za uendelezaji wa jengo a Terminal II.
2. Kamati inaiomba Serikali na Wizara ya Fedha kwa ujumla kuharakisha uwekaji wa 'transformer' katika Kiwanja cha Pemba ili huduma zitakazotolewa ziwe za uhakika na endelevu.
3. Pia, Kamati inaishauri Serikali pamoja na Wizara kupitia Mamlaka ya Uwanja wa Ndege kuharakisha ununuzi wa kifaa cha kuongozea ndege (ILS) katika Uwanja wa ndege wa Kimataifa AAKIA hali ambayo itaongeza pato la Taifa kupitia Sekta hii ya usafri wa Anga.
4. Kamati inaiomba Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka kuendelea na ukarabati wa jengo na sehemu za kushukia na kuondokea abiria wakati wa safari zao ili kupunguza hali ya msongamano ambayo hupelekea upotevu wa mizigo kwa baadhi ya siku hususan ukizingatia siku ya Jumatano.
5. Kamati inaiomba Serikali na Wizara kuweza kutafuta njia mbadala ya kuwapatia Mamlaka ya Uwanja wa Ndege kikosi cha Zimamoto cha kudumu.

2:12:00 SEKTA YA MAWASILIANO

2:12:02 IDARA YA MAWASILIANO

Idara ya Mawasiliano Zanzibar inajukumu la kusimamia huduma ya mawasiliano pamoja na technolojia ya habari. Aidha, Idara inajukumu pia la kuratibu masuala ya Taasisi za Mawasiliano za Serikali.

2:12:03 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI IDARA YA MAWASILIANO

1. Elimu ndogo juu ya matumizi ya TEHAMA kwa wananchi.
2. Huduma za mtandao (internet) katika baadhi ya maeneo zimekua shida kutokana na kukosekana kwa miundombinu bora ya internet za uhakika.
3. Ukataji wa mkongo wa Taifa kwenye baadhi ya maeneo yanarudisha nyuma uwezo wa kuendeleza Mkonga huo na maendeleo ya nchi kwa ujumla.
4. Ukosefu wa Sheria ya ICT ambayo itaweza kusimamia Sera ya Mawasiliano hapa Zanzibar.

2:12:04 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaiomba Serikali kwa kushirikiana na Wizara kuendelea kuimarisha miundombinu ya mawasiliano ili kuweza kuwa na uwezo mkubwa na hivyo kuweza kubeba habari picha na habari data ili kufikia maendeleo endelevu ya Dunia.
2. Kamati inaiomba Serikali na Wizara kwa ujumla iwashirikishe wadau wote kabla ya kuanza kuekeleza miradi inayojipangia hususan katika masuala mazima ya mawasiliano.

2:12:05 KAMPUNI ZA SIMU ZA MKONONI

Wakati wa kazi za kamati, Kamati pia ilitembelea Baadhi ya Mashirika na Kampuni za Simu za mkononi pamoja na Shirika la Posta hapa Zanzibar.

2:12:06 CHANGAMOTO ZINAZOZIKABILI KAMPUNI ZA SIMU ZA MKONONI

a. Baadhi ya Makampuni yanalalamikia urasimu mkubwa wa kupatiwa vibali vya ujenzi na utandikaji wa miundombinu yao ili kuweza kuwafikia wateja wao sehemu zote hapa nchini.(Mfano, Kampuni ya halotel).
b. Ushindani usiokua wa lazima baina ya Makampuni yanayotoa huduma za mawasiiano ya simu za mikononi na kuharibiana mipango ya maendeleo ya kampuni hizo.

2:12:07 MAFANIKIO

Aidha, pahali popote duniani panapokuwa na changamoto hapakosi pia kuwa na mafanikio. Makampuni ya simu za mkono ni moja ya chanzo kinachoingiza mapato makubwa kwa Serikali yetu ya Zanzibar. Miongoni mwa mafanikio hayo ni kama yafuatayo:-

1. Kampuni za Mawasiliano ya simu zimekuwa zikilipa kodi zao vizuri serikalini na kusaidia kuongeza pato la Taifa.
2. Kupunguza tatizo la ajira kwa ajira ya moja kwa moja (Direct) au japo sio moja kwa moja (indirect).
3. Kuisaidia huduma mbai mbali za kijamii kama vile afya

2:12:08 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inayaomba Makampuni kuunganishwa haraka kwa mikongo ya Taifa ili kupata njia mbadala ya ambayo itabeba mzigo mkubwa wa mawasiliano.
2. Kamati inayaomba Mkampuni ya simu za mkononi kufikiria kuweka huduma ya “Free Wifey” katika maeneo ya wazi ya “Public’ kama vile Hospitali kuu ya Mnazi Mmoja, Forodhani, Michenzani na maeneo mengine yanayofanana na hayo ili kuzidi kuwasaidia wananchi kufaidika na huduma ya “WIFEY”.

2:12:09 SHIRIKA LA POSTA ZANZIBAR

2:12: 10 CHANGAMOTO ZINAZOZIKABILI SHIRIKA LA POSTA ZANZIBAR

1. Muingiliano wa Sheria za Zanzibar na za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hususan katika utekelezaji wa kazi zetu mfano wa Sheria ya Uvuvi wa baharini na Uuzaji wa baadhi ya mazao ya bahari imekuwa ni moja ya chngamoto zinazotukabili. Sheria ya Zanzibar inaruhusu usafirishaji wa majongoo ya baharini wakati ile ya Muungano hairuhusu.
2. Kutotambulika kwa baadhi ya vibali vya taasisi za Zanzibar vifikapo Tanzania Bara, mfano Taasisi kama ya Mkemia Mkuu, Bodi ya Chakula na Dawa nk. Kadhia hii husababisha mizigo kuzuiliwa ifikapo Uwanja wa ndege wa Dar es Salaam huku watendaji wa taasisi za Tanzania Bara wakidai kuwa Zanzibar haitambuliki kimataifa na kutaka vibali hivyo vichukuliwa katika taasisi zao ziliopo Tanzania Bara.
3. Mwamko mdogo wa huduma za Posta kwa Ofisi za SMZ. Hali ambayo hupelekea kukosa wamtumiaji wa huduma hizo kwa wakati na pia kuikosesha Serikali pato.

2:12:11 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaiomba Serikali ifanye juhudi za kuhakikisha kwamba inaweka utaratibu wa kutatua kero ya kutotambulika kwa vibali vya Taasisi za Zanzibar kwa wakuu wa Taasisi hizo ambazo si za Muungano kuweka utaratibu unaoeleweka ili wananchi waweze kupata huduma za kiposta bila ya usumbuvu wowote.
2. Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Makampuni kutoa elimu kwa watumiaji wa huduma hizo pamoja na taasisi za serikali juu ya umuhimu wa kuzitumia huduma hizo ipasavyo.

SEHEMU YA TATU

3:0 HITIMISHO

Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi inawashukuru sana Watendaji wote wa Wizara pamoja na Taasisi zote za Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii kwa kuweza kutoa mashirikiano makubwa ya kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa mwaka huu. Kamati inashauri mashirikiano hayo yaendelezwe kwa kipindi chote kinachofuata.

Hata hivyo, kasoro kubwa iliyogunduliwa na Kamati ni **Upatikanaji wa fedha na kwa wakati na pia kwa kiwango kilichokadiriwa kutoka serikalini** kumekwamisha kwa kiasi kikubwa malengo na shabaha za Wizara zote mbili zinazosimamiwa na Kamati hii hasa katika miradi ya Maendeleo.

Vile vile, upatikanaji wa fedha za OC pamoja na vitendea kazi, usafiri na malipo ya muda wa ziada wa kazi (overtime) navyo vimekuwa virejesha nyuma mwamko na ufanisi wa kazi.

3:1 MAPENDENDEKEZO NA MAAGIZO YA KAMATI KWA SERIKALI

- Kamati inaiagiza Serikali kuzipatia Wizara hizi fedha za Bajeti kwa wakati.

  Aidha Kamati inatoa shukurani za pekee kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Katibu na Watendaji wote wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mzuri.